



**TALKING NOTES ZA MHE. THOBIAS E. M. ANDENGENYE, MKUU WA MKOA
WA KIGOMA WAKATI AKIZUNGUMZA NA WAJUMBE WA BARAZA LA
MADIWANI LA HALMASHAURI YA MANISPAA KIGOMA/UJIJI
TAREHE 11 DESEMBA, 2021**

UTANGULIZI

Mhe. Baraka Naibuha Lupoli - Mstahiki Meya wa Manispaa,

Kamati ya Usalama ya Mkoa

Mhe. Ester Alexander Mahawe - Mkuu wa Wilaya,

Mhe. Mgeni Omari Kakolwa - Naibu Meya wa Manispaa,

Ndg. Athuman Msabila - Mkurugenzi wa Manispaa,

Ndg. Yassin Mtalikwa - Mwenyekiti wa CCM wa Wilaya,

Ndg. Viongozi wa Vyama vya Siasa,

Ndg. Wajumbe wa Kamati ya Usalama ya Wilaya,

Wah. Madiwani,

Ndg. Watendaji katika ngazi mbalimbali,

Ndg. Wageni Waalikwa,

Ndg. Waandishi wa Habari,

Mabibi na Mabwana.

Nawasalimu kwa Jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania!



Waheshimiwa Madiwani,

- Natoa Shukrani kwa Uongozi wa Wilaya ya Kigoma na Halmashauri ya Manispaa Kigoma/Ujiji kwa Mwaliko wa kushiriki katika Mkutano huu Malaalum.

Wahe. Madiwani,

- Niwapongeze kwa kufikia maamuzi sahihi katika Mkutano huu, maamuzi yenyе lengo la kupiga hatua ya kuwaleta maendeleo wananchi wa manispaa ya Kigoma Ujiji.
- Niwaombe katika hatua ambayo mmeshafikia, nendeneni mkavunje makundi ya uchaguzi wa Meya ili nyote mkawe kitu kimoja na kuacha kulumbana. Malumbano hayana faida kwa wananchi waliowatuma kusimamia maendeleo.
- Niwakumbushe kufuata taratibu zinazo ongoza Mabaraza na Mamlaka za Serikali za Mitaa pale mnapona uwepo wa dosari za kiutendaji tukifanya hivyo Manispaa yetu itapaa kimaendeleo.
- Mkurugenzi wa Manispaa angalia uwezekanao wa kuandaa mafunzo kwa waheshimiwa Madiwani yanayouhusu Uongozi na Utawala, mnaweza kuwaita wataaalamu kutoka Vyuo vya Seriklai za Mitaa Hombolo waje kutoa somo kwa waheshimiwa.



- Manispaa ya Kigoma Ujiji ni kioo katika Mkoa wetu hivyo tunategemea Halmshauri nyingine zifunze kutoka Manispaa ya Kigoma Ujiji namna yta uendeshaji, ukusanyaji Mapato, usimamizi wa fedha na miradi na maendeleo kwa ujumla.
- Nendeni mkajikite kuweka msisitizo wa kuimarisha usimamizi wa vyanzo vya mapato na ufuatiliaji wa makusanyo. *Kuweni wabunifu na ibueni vyanzo vinya vya mapato.*
- Boresheni utoaji huduma na tatuensi kero za Wananchi kwa wakati.
- Zibeni mianya yote ya upotevu wa mapato. Manispaa inapoteza mapato mengi kutohana na udhaifu mkubwa wa baadhi ya Watendaji na mifumo ya ukusanyaji isiyosimamiwa vizuri.
- Mwisho kabisa ninyi ni wawakilishi wa wananchi, wekeni pemberi maslahi binafsi tangulizeni maslahi ya wale waliowatuma kuwawakilisha.

Akhsanteni kwa Kunisikiliza.